*Kioo cha Lugha* 2, 1996/97:81-99

# Nadharia ya Fasihi na Fasihi ya Kiswahili ya Majaribio

*F.E.M.K. Senkoro**

## Utangulizi

Makala hii inajaribu kupitia baadhi ya nadharia za uhakiki na upokeaji wa kazi za fasihi. Mkazo umewekwa katika nadharia kuu tatu za hivi karibuni: Umundo, Finominolojia na Hemetiki. Nafasi ya nadharia hizi katika upokezi na uhakiki wa kazi za fasihi inajadiliwa. Katika kufanya hivyo, mawazo ya waasisi wakuu wa nadharia hizo yanachambuliwa.

Sehemu ya pili inajaribu kuonyesha athari za mawazo na falsafa zitokanazo na nadharia hizo katika utungaji wa fasihi ya Kiswahili. Hapa tunamtumia E. Kezilahabi kuwa kielelezo cha athari hizo kwa kuchambua baadhi ya kazi zake za fasihi, hasa za hivi karibuni ambazo ni za majaribio.

Madhumuni makuu ya makala hii ni kuona ni misingi gani na nguvu zipi za kijamii zinazoibusha na zinazoendelea kuainisha nadharia na falsafa za mikururo mbalimbali ya fasihi na za ubunaji wa kazi za fasihi.

## Mhakiki Adili

Mitazamo mbalimbali kuhusu mhakiki adili imejitokeza katika nyakati tofauti tangu enzi za wanafalsafa wa mwanzo kama vile wa Kigiriki na Kirumi, mathalani akina Socrates, Plato na Aristotle, hadi leo. Hii haikutofautiana tu kutoka wakati hadi wakati, bali hata baina ya wahakiki hawa na wale hata kama wote ni wa mahali na wakati mmoja. Mitazamo hii aghalabu imeathiriwa na kukuzwa na mabadiliko ya kazi za fasihi, nadhari mbalimbali za kazi hizo na hata uwanja wenyewe wa tahakiki.

Mambo yote haya tunayaona, kwa mfano, katika mkusanyo wa tahakiki na nadharia mbalimbali zilizomo katika kitabu cha James Harry Smith na Edd Wienfield Parks, *The Great Critics.*[1] Hizi tumezipa nafasi yake mahsusi katika makala.

---

* Profesa Mshiriki, Idara ya Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam

Nao Mills Gayley na Fred Newton Scott, katika *Methods and Materials of Literary Critics*[2] wametoa vielelezo vya mitazamo mbalimbali kuhusu mhakiki adili atakiwaye. Kielelezo cha kwanza humwona mhakiki kwa "jicho la jadi" kuwa yeye ni *mtafuta makosa*. Jukumu la mhakiki huyu basi, ni kutafuta udhaifu wa kazi ya fasihi na kuudhihirisha kwa hadhira. Huyu anayafungia macho mambo yote mazuri ya kazi ya fasihi kwani hayo yanadhaniwa kuwa ni ya kawaida mno kwake yeye na kwa hadhira ya kazi yake.

Mathew Arnold alijaribu kuupa uhakiki wa fasihi mtazamo huohuo ijapokuwa aliupanua zaidi. Yeye pia alimwona mhakiki kuwa ni mtu anayekosoa badala ya kusifu. Alipingwa na wataalamu wengineo kama vile akina Moulton na Taine ambo walidai kuwa mhakiki adili hana budi kutafuta na kuupanua uzuri wa kazi ya fasihi na kuielimisha jamii juu ya uzuri huo. Wakati huo huo wapo baadhi ya wataalamu ambao walimwona mhakiki adili kuwa ni yule anayeiangalia kazi ya fasihi bila kutaja juu ya ubaya au uzuri wa kazi hiyo.

Mtazamo mwingine kuhusu mhakiki adili ambao vilevile ulitajwa na Gayley na Scott umeelezwa pia na Philo M. Buck Jr., katika kitabu chake cha Literary Criticism. Huu humwona mhakiki kuwa ni Hakimu atoaye hukumu. Ni mtazamo ambao hautofautiani sana na wa Plato. Anasema Buck Jr. haya yafuatayo kuhusu mhakiki huyo:

> He is a mana who reads to pronounce judgement, who owing to his assumption of a judicial air and robes can not allow his mind to be swayed by trifles; who can't stoop so low as to enjoy with uncritical pleasure the book against which he must utter a sentence.[4]
>
> *(Ni mtu asomaye ili atoe hukumu kuhusu kazi ya fasihi, ni msomaji ambaye kutokana na uanasheria ajipao pamoja na joho la Jaji analolivaa, hairuhusu akili yake kuyumbishwa na mambo madogo madogo; hakubali kujishusha chini mno kwa kuifurahia kazi ya fasihi bila jicho kali la kutolea hukumu aliyoidhamiria).*

Mtazamo huu hautofautiani na namna Plato alivyoiona kazi ya fasihi/sanaa na uhusiano wake na hisia na jaziba za watu dhidi ya uwezo wao wa kutumia akili katika kuikabili kazi hiyo.[5]

Aina nyingine ya mtazamo juu ya mhakiki adili imetolewa na J.M. Robertson katika kitabu chake cha *Essay Towards A Critical Method*.[6] Katika insha hii ndefu, mhakiki adili anahitajiwa awe mlinganishaji. Robertson anasema haya kuhusu uhakiki:

> Criticism is a process that goes on over all the field of human knowledge being simply comparison or clash of opinion.[7]
>
> *(Tahakiki ni mwenendo unaoshughulikia nyanja zote za maarifa ya mtu; na, kwa hakika, huwa ni mlinganisho au mgongano tu wa kauli).*

Mawazo haya yanakaribiana sana na yale ya mtaalamu wa zamani sana, Dionysius wa Halicarnassus aliyeishi katika miaka ya 50 Kabla ya Masihi. Huyu hata katika tahakiki zake alifuata mkabala wa kiulinganishi badala ya ule wa kiumbuji (rhetoric) wa wahakiki waliomtangulia. Akitumia msingi huu, Dionysius katika tahakiki zake alichunguza na kuchambua mitindo ya waandishi wengine huku akionyesha kuwa mtindo wa kiumbuji ulikuwa na udhaifu mwingi kwani uliiona kazi ya fasihi katika upekee na upweke mno bila kuihusisha na nyanja zingine.

Mawazo sawa na ya Dionysius tunayakuta yakijitokeza baadaye, kwa namna fulani, katika andiko la Longinus, *On the Sublime*.[8] Andiko hili liliasi mtindo wa kiumbuji wa kuhakiki kazi za fasihi, nalo liliorodhesha vipengele kadhaa vya kufuatwa wakati wa kuhakiki kazi ya fasihi. Kati ya hivyo, Longinus alisisitza vile vya uzito wa maudhui, undani wa mawazo, matumizi ya tamathali za semi, uchaguzi mzuri wa maneno na matumizi mufti ya lugha kwa jumla.

Tumrejelee, Mathew Arnold, tuliyemtaja hapo juu, ambaye alimweleza mhakiki adili kuwa ni yule "aonaye jambo kama lilivyo hasa." Ijapokuwa kifalsafa maelezo haya yanaweza kupanuliwa na baadhi ya wataalamu, yanaibusha maswali mengi zaidi kuliko majibu kuhusu mhakiki/uhakiki adili. Hapa tunajiuliza, kwa mfano, kama kuna tofauti yoyote baina ya Arnold na wale waliouona uwanja huu kuwa ni mahakama itoayo hukumu kuhusu kazi ya fasihi. Hapo hapo, kuliona jambo "kama lilivyo hasa" huweza kupatikana kutokana na ulinganishi. Kama hivyo ni sawa basi, ni mambo gani mawili au zaidi yaliyo sawa sawa na ambayo yanaweza kulinganishwa, hasa tutiliapo maanani ukweli kuwa hakuna mambo mawili, hasa tunapoongelea kazi za fasihi/sanaa, yanayoweza kufanana kabisa? Je, katika maelezo haya ya Arnold, tuweke wapi masuala ya hukumu, kufurahia, kutoa makosa na mengineyo kama hayo?

Katika kitabu cha Smith na Parks tulichokitaja, aina kuu tatu za wahakiki zinaibuka. Kwanza twaelezwa kuwa kuna wahakiki wa *kimamlaka*. Wengi wao ni wale wa Kirasimi na Kiurasimi Mpya.[9] Smith na Parks wamewaelezea hawa kuwa ni mabingwa ambao wanatazamiwa, katika kuhakiki kwao, watoe maandiko na matamko ya kimamlaka:

> Here the ideal critic is a technochrat,.... One who is supposed to delve deep into producing technical treatises.[10]
>
> (Humu, mhakiki adili ni fundi stadi mwenye mamlaka, anayetegemewa azame ndani haśa na kuibuka na maelezo ya kitaalamu).

Smith na Parks wanaieleza aina nyingine ambayo inafanana na hiyo kuwa ni ya wale watumiao akili (reason) katika kuikabili kazi ya fasihi, na tahakiki zao huzama kiuchambuzi hata kama wao wenyewe si mabingwa wa uwanja wanaoushughulikia. Aina ya tatu ni ile ya wahakiki wanaosisitiza kuhusu vionjo vya hadhira ya kazi ya fasihi. Hawa basi, daima hufikiria kwanza kuhusu aina ya hadhira na vionjo vya hadhira hiyo kabla ya kuichambua kazi ya fasihi.

Kwa jumla tunaweza kuongelea aina kuu mbili za wahakiki ambazo zimejitokeza katika historia ya uhakiki wa kazi za fasihi: wahakiki wa kihakimu, na wale ambao huchambua kazi hizo katika mapana na marefu yake na kutoa kauli za kitaalamu kuhusu kazi hizo. Kwa Kiingereza, hawa wa pili huitwa *Inductive Critics.* Kuhusu aina ya kwanza ya wahakiki, vigezo wanavyovisisitiza ni vya hukumu. Hivyo huchambua na kutathmini ili kujaribu kuvumbua na kuonyesha uzuri au ubaya wa kazi ya fasihi. Aina ya pili imehusisha zaidi utafutaji wa mambo muhimu ya fani na maudhui yanayoibuka katika kazi ya fasihi. Mhakiki wa namna hii hukataa kutathmini au hata kuvumbua uzuri wa kazi ya fasihi kabla ya kujishughulisha na maelezo ya hatua kwa hatua ya maudhui na fani ya kazi hiyo ya fasihi.

Wakati mwingine mhakiki huyu anapevuka zaidi kwa kuichukulia kazi ya fasihi kuwa ni kielelezo cha athari mbalimbali za kimazingira. Kwa hiyo basi, mhakiki huyu huthamini sana na hutilia maanani katika kazi zake, masuala ya kisiasa, kitamaduni na kiuchumi, na jinsi yanavyoathiri na kuijenga kazi ya fasihi. Mhakiki huyu pia huamua kuhusu kazi Fulani ya fasihi kwa kuilinganisha na kuilinganua na kazi zinginezo za aina hiyo, za wakati huo na zinazotokana na mazingira hayo hayo.

Msimamo huo wa uhakiki ni msingi mkuu wa uhakiki wa Ki-Marx. Huu huichambua kazi ya fasihi kwa kuihusisha na nguvu mbalimbali za jamii ambazo ndizo zilizoizaa kazi hiyo. Katika kufanya hivyo, uhakiki wa Ki-Marx husisitiza pia masuala ya *ITIKADI,* hasa kuhusu utabaka wa watu katika jamii na athari zake katika uundaji wa kazi ya sanaa; kwani, kufuatana na uhakiki huu, kila msanii ni mwakilishi wa tabaka fulani, kwa kupenda au la, kwa kujua ama kutokujua.

**Umundo, Finominolojia na Hemetiki**

Hata hivyo kuna mkururo wa mawazo na wa nadharia ya sanaa ambao unapinga sana mtazamo huu wa kuiangalia kazi ya fasihi kwa kuihusisha na hali za kijamii. Huu ni wa *Umuundo* ukishirikiana na ule wa *Kifinominolojia*.[11] Kwa vile mkururo huu ndio mtindo wa nadharia na tahakiki ambao leo hii umetawala hasa katika nchi za Magharibi, nitauongelea kwa kirefu kidogo humu. Katika mkururo huu inadaiwa kuwa kazi ya fasihi ni "kiumbe" kinachojitegemea chenyewe, chenye urazini wake na ulimwengu wake *ndani* yake. Wawakilishi wakuu wa mawazo ya aina hii ni, hasa, Edmund Husserl na Martin Heidegger.[12]

Kwa Husserl, kwa mfano, nguvu mbalimbali za historia zilizomzaa na kumlea mwandishi, nguvu ambazo ndizo pia zinazaa na kuathiri kazi mbalimbali za fasihi pamoja na hadhira zake, zote zinatupiliwa kando. Badala yake Husserl anadai kuwa kuna ubikra wa kazi za fasihi, "uhai" wa riwaya, shairi ama tamthilia, ambao kamwe hauathiriwi na nguvu zozote za nje.

Uhakiki wa Kimundo na Kifinominolojia basi, humuona msanii kuwa ana urazini wa pekee, urazini ambao hujitokeza katika kazi yake ya fasihi; na maana ya kazi hiyo ya fasihi hubaki ikiwa imegandamana katika urazini huo ndani ya kazi hiyo bila kubadilika ama kuyumbishwa na nguvu zozote za nje. Kutokana na mawazo haya basi, kila kazi ya fasihi ina mtindo na maana ambavyo hushirikiana katika kujijumlisha ili kutoa urazini wa kazi yenyewe kwa kupitia katika "ndani" wa msanii. Undani huu, zinaeleza nadharia za Finominolojia, ni wa pekee kwa mwandishi, nao hauna uhusiano wowote na mazingira ya nje. Kwa hiyo, ili kuijua maana ya kazi ya fasihi, hadhira inaonywa isije ikaihusisha kazi hiyo na jambo lolote inalojua kuhusu maisha ya mwandishi. Uhakiki wa kibiografia umepigwa marufuku kabisa katika mtazamo wa Kifinominolojia. Tunalotakiwa kufanya ni kuvivumbua vile vigezo vya kazi ya fasihi vinavyoibua "urazini wa ndani" wa msanii. Hapa basi, msisitizo umewekwa katika "miundo ya ndani" ya kazi ya fasihi, miundo ambayo twaelezwa kuwa hujitokeza katika TASWIRA na DHAMIRA zinazoibuka mara kwa mara katika fasihi ya mwandishi fulani kiasi kwamba humo tunaweza kung'amua namna mwandishi alivyoishi katika ulimwengu wake.

Uhalisi, kufuatana na nadharia hizi, si ule unaojenga taswira na dhamira za kazi ya fasihi kutokana na nguvu za kijamii za uchumi, siasa na utamaduni, bali ni aina ya uhalisi ujulikanao kwa Kijerumani kama *Lebenswelt*. Ni uhalisi

unaoasilishwa, unaoundwa na kuenezwa na mtu mwenyewe, mmoja mmoja, katika *unafsi* na *undani* wake.

Kutokana na mawazo haya, uhakiki wa fasihi hauonekani kamwe kuwa wa kufasili na kutoa maana ya kazi ya fasihi kijamii. Mhakiki hapa anatakiwa awe *mpokeaji* wa kazi ya fasihi asiyeuliza maswali wala kuchokonoa kuhusu uhusiano baina ya kazi hiyo ya fasihi na jamii. Mhakiki anatakiwa aione kazi ya fasihi ya mwandishi mmoja kuwa ni kiumbe chenye sifa fulani za pekee. Hata kazi mbalimbali za mwandishi, kazi ambazo huenda ziliandikwa katika nyakati tofauti tofauti kushughulikia masuala yanayotofautiana, zatakiwa zote zichambuliwe kama *kiumbe* kimoja.

Namna suala la lugha linavyojadiliwa na kukabiliwa na wanafinominolojia ni jambo lingine linaloonyesha msimamo wao. Katika jitihada za kuhubiri "ubikra" na "uasili" wa vitu, lugha ya maneno kwa mtazamo wa Kifinominolojia, haina umuhimu wowote wala uzito katika kazi ya fasihi. Kwa Husserl, lugha ya maneno inasaidia tu kwa kiasi kidogo sana kuibusha maana ya undani wa kazi ya fasihi. Kwa maneno mengine, lugha hii si nyenzo muhimu katika kutoa maana ya kazi ya fasihi. Badala yake, Husserl anaongelea "Uzoefu wa kibinafsi na wa ndani" ujitokezao katika kazi hiyo ya fasihi. Ijapokuwa ni vigumu sana kufahamu namna uzoefu wa aina yoyote unavyoweza kujidhihirisha bila lugha, Husserl haonekani kughasiwa na jambo hili. Yeye na wafuasi wake hujaribu kuitupilia kando lugha, kwani kwao lugha hiyo ni mojawapo ya "uchafu" wa athari za kijamii ambazo Wanafinominolojia huchukia kuziona zikihusishwa na kazi takatifu za fasihi.

Martin Heidegger ndiye mfuasi mkuu wa Husserl ambaye, ijapokuwa alijaribu kuvunja miiko ya mwalimu wake kwa kuhusisha maana ya kazi ya fasihi na uhalisi wa nguvu za kihistoria katika jamii inayohusika hatimaye mtazamo wake uliangukia kule kule kwa muasisi wa Finominolojia. Katika andiko lake la *Being and Time*[13] Heidegger anachunguza suala la kuwako, suala la uhai wa mtu. Ijapokuwa anakubali kuwa lugha ni jambo muhimu na la msingi katika kuwako kwa jamii, bado Heidegger anaiona lugha sawa na vile mwalimu wake anavyoiona kazi ya fasihi, kuwa ni "kiumbe" chenye kujitegemea kwa uhai wake. Lugha basi, iko nje na kando ya jamii, nao wanajamii huichota tu na kuitumia. Lugha inaishi maisha ya pekee ambayo huifanya jamii ya watu ikamilike ijapo na kujidhihirisha ndani ya lugha hiyo.

Kutokana na mawazo ya Heidegger, ilizuka nadharia ya hemetiki[14] ambayo hali kadhalika imetumiwa sana katika kuhakiki kazi za fasihi. Kwayo

ilizaliwa Finominolojia ya Kihemetiki ambayo athari yake kubwa inajitokeza katika kazi ya mwanafalsafa wa Kijerumani, Hans-Georg Gadamer, ya Truth and Method.[15] Katika kazi hii Gadamer anauliza maswali muhimu manne:

(a) Ni nini maana ya kazi ya fasihi?
(b) Je, maana hii inahusianaje na kusudi au lengo la mwandishi?
(c) Je, tunaweza kuzielewa kazi za fasihi za tamaduni na historia tofauti na zetu?
(d) Je, ni rahisi kupata uelewaji wa ndani wa kazi ya fasihi au huu hutegemea mazingira na historia ya hadhira inayohusika?

Katika kujaribu kuyajibu maswali haya, wanafinominolojia ya kihemetiki wanadai kuwa maana ya kazi ya fasihi huwa tayari imo ndani ya kazi hiyo, haibadiliki daima dumu. Inalandana na undani wa unafsi na urazini wa mwandishi wakati alipoitunga kazi h Mtazamo huu ni sawa na wa mwanahemitiki wa Kimarekani, E.D. Hirsch Jr. unaojitokeza katika kazi yake ya *Validity in Interpretation*[16], nao umeelezwa na Terry Eagleton kama ifuatavyo:

> It does not follow for Hirsch that because the meaning of a work is identical with what the author meant by it at the time of writing, only one interpretation is possible. There may be a number of different valid interpretations bu all of them must move within the system of typical expectations and probabilities which the author's meaning permits.[17]
>
> *(Kwa Hirsch, si lazima kuwa kwa vile maana ya kazi ya fasihi hulandana na ile aliyoikusudia mwandishi/mtunzi wakati wa kutunga, basi fasili moja tu ya kazi hiyo ndiyo sahihi. Inawezekana kuwa na fasili aina aina, lakini zote hazina budi kukaribia matarajio na matazamio ambayo maana ya mwandishi yaruhusu)*

Nadharia za Kifinominolojia zinadai kuwa fasili tofauti tofauti zinazotolewa na wasomaji mbalimbali wa kazi moja ya fasihi katika nyakati tofauti zinaashiria tu tofauti za msisitizo na umuhimu wa kazi fulani kwa watu hao. *Maana* hasa ya kazi hiyo hubaki kuwa ileile. Inashangaza ni kwa vipi *umuhimu* wa kazi ya sanaa utaibuka na kubadilika bila kuhusishwa na maana ya kazi hiyo.

Kwa mawazo ya Hirsch, maana iliyomo ndani ya kazi ya fasihi haitokani hasa na lugha, bali inaimliwa na mtunzi. Maana hiyo ni lidubwana lisilo na lugha, nalo linatokana na linaasilishwa na urazini wa kazi yenyewe. Ni lidubwana ambalo limekakawana mumo humo daima dumu, na halina maneno ya kulidhihirishia.

Ijapokuwa inakuwa vigumu hata kuwaza ni kwa vipi maana na hata huo urazini wenyewe huweza kuwapo bila lugha, hili halimghasi Hirsch. Gadamer alijitahidi kuihusisha kazi ya fasihi na historia ili kujaribu kukwepa utata unaotokana na mkabala wa Ki-Hirsch, historia hiyo iliyoelezwa kuwa iliunganisha yaliyopita, yaliyopo na yajayo, ilirudishwa kule kule kwenye udubwana wa Ki-Hirsch, kwani ilitenganishwa na athari mbalimbali za migongano na mivutano ya kijamii.

*Nadharia ya Upokezi (Reception Theory)* au *Ujumi wa Kipokezi* ni mtindo wa hivi karibuni wa Kihemetiki. Nadharia hii ni muhimu kwani inakiri na kutambua nafasi muhimu ya HADHIRA. Wakati ambapo nadharia zilizoitangulia hii ya Ujumi wa Kipokezi zilisisitiza mno kuhusu ama mtunzi au kazi yenyewe ya fasihi, hii inatangaza kuwa bila hadhira kazi za fasihi zisingekuwapo kwani hazitungwi ili zihifadhiwe katika mashubaka ndani ya maktaba, bali zinaandikwa ili zisomwe na hadhira.

Nadharia ya Upokezi basi, inajaribu kuchunguza tendo la USOMAJI, tendo ambalo pia limemshughulisha sana mwananadharia maarufu wa Poland, Roman Ingarden.[18] Huyu aliiona kazi ya fasihi kuwa ina matabaka matabaka yenye kuelekeza pande mbalimbali ili msomaji aikabilipo aipe welekeo mahsusi.

Kitendo cha usomaji, kwa nadharia ya upokezi, kinamwona msomaji kuwa ni mtu anayekuja na dhana, imani na amali ambazo hurekebishwa ama kuthibitishwa na yale yaliyomo ndani ya kazi ya fasihi. Msomaji anachuja kati ya hayo na kuyapanga yale yanayomtukia kuwa ya maana kwake.

Twaelezwa na wafuasi wa tawi hili la Hemetiki kuwa katika tendo la usomaji kuna *mviringo wa ki-hemetiki* ambao unamfanya msomaji aende mbele na nyuma, kushoto na kulia kwa yale yaongelewayo katika kazi ya fasihi. Kitendo cha kusoma na kuhakiki ni cha kuiangalia kazi ya fasihi katika uchangamano wake wa mbele na nyuma. Hadhira huwa wanabashiri na kuhusisha mambo wanayoyakuta humo na yale waliyokwisha kuyapitia maishani mwao.

Haya yote na mengine yameelezwa na Wolfgang Iser katika kitabu chake cha *The Act of Reading* ambamo anasisitiza kuwa ili kuweza kuisoma kazi ya fasihi kikamilifu, lazima msomaji aelewe mbinu za kifasihi pamoja na ada au kanuni na kawaida zinazotumika humo.

Kwa hakika, analomaanisha Iser hapa ni kuwa kuna *sheria* zinazofungamana na utolewaji wa maudhui na thamani zilizojificha katika urazini wa msanii ndani ya kazi ya fasihi. Kazi ya hadhira basi, ni kuzimaizi fika sheria hizo. Sheria hizo huambatana na muktadha, yaani zile nguvu za kijamii zinazochangia katika kuunda huo urazini wa msanii. Iser na wafuasi wake wanajitahidi, hata hivyo, kuzigandamanisha sheria na nguvu hizo mumo humo ndani ya kazi ya fasihi na kudai kuwa hizo ndizo zinazomsukia na kumuibukia msomaji anapoikabili kazi yoyote ya fasihi. Kwa mawazo ya Iser, msomaji adili ni yule anayeikabili kazi hiyo bila kuwa na mawazo, imani na msimamo *mkali* mwanzoni. Anahitajiwa aijie kazi ya fasihi kimbumbumbu, na umbumbumbu wake uondolewe na ayakutayo humo. Hii ina maana kuwa hata baada tu ya msomaji huyo huyo kumaliza kuiangalia kazi hiyo, anahitajiwa ayasahau yote aliyoyapata humo anapoikabili kazi nyingine ya fasihi, na aurudie umbumbumbu wake wa mwanzo.

Haya yote na mengineyo ya aina hii yanayojitokeza katika nadharia hizi za mitazamo ya Umundo, Finomonolojia, hemetiki na Upokezi, tuyachukulieje katika uwanja wa tahakiki?

Katika nadharia hizi inadaiwa kuwa lugha ya maneno imepigwa vikumbo na maendeleo ya urazini wa mtu kiasi ambacho *ishara* pekee ndiyo mbinu ya kuuelezea *ukweli*. Inadaiwa kwa mfano, kuwa mwanasiasa anapochemka katikati ya hotuba ya kuwahimiza watu wawe na umoja na wazalishe mali kwa wingi, halafu ghafla akiwa na *kituo* kabla ya kuendelea na hotuba yake, basi kituo hicho ndicho cha maana sana kuchambuliwa kuliko hotuba yenyewe. Na inasisitizwa kuwa *umaana* wa kituo usije ukahusishwa na lugha ya maneno bali uangaliwe *kiishara*. Ijapokuwa ni vigumu kuwaza kuhusu ishara isiyo na uelezwaji au uelezekaji kwa kupitia katika nyenzo ya lugha ya maneno, nadharia hizi hazielekei kushangazwa na jambo hili.

Misingi ya nadharia hizi ni udhanifu unaojaribu kukwepa uhalisi wa nguvu za kijamii za uchumi, siasa na utamaduni. Zimejikita katika kuikwepa historia ya jamii iliyo chanzo na mwisho wa sanaa yoyote ile, ikiwemo fasihi. Ni matokeo ya mfumo wa jamii wa kibepari unaojidhihirisha katika itikadi mufilisi zinazojitahidi kuhubiri kuhusu miliki za kibinafsi ambazo zinanuia kwa hali yoyote ile kuidhanifisha kazi ya fasihi na kuifanya kazi hiyo iwe ni mali ya mwandishi tu. Ndiyo maana kwa Hirsch na wafuasi wake inawabidi waandike nadharia ndefundefu za mzunguko za kujaribu kudhihirisha kuwa hata maana inayojitokeza ndani ya kazi ya fasihi ni mali takatifu ya

msanii, ni mali ya kibinafsi ambayo haina budi kulindwa isije ikaangukia mikononi mwa msomaji. Maana hii yatakiwa ionekane kuwa ni *siri* ya ndani ya mwandishi ambayo kamwe haiwezi kutolewa hadharani na kufanywa kuwa mali ya hadhira.

Kwa nini basi hata lugha idhanifishwe? Kwa wanafinominolojia uko mkabala wa kuiogopa lugha, kwani kukiri kuwa lugha ni kitu cha kijamii, na kwamba ni matokeo ya kuwapo kwa jamii ya watu, hapo hapo tutakuwa tunakiri kuwa inavyotumika katika kazi ya fasihi huibusha masuala ya kijamii, ukweli ambao ni mwiko katika misingi ya nadharia hizi.

Nadharia hizi zinaiona kazi ya msomaji kuwa ni ya *kupokea* tu. Lakini tujuavyo, msomaji/mhakiki adili ni mwanafunzi na mwalimu kwa wakati huo huo anapoikabili kazi ya fasihi. Anatumia ujuzi wake wa taaluma mbalimbali, pamoja na wa historia ya jamii ya mwandishi na ya mwandishi mwenyewe ili kuona jinsi kazi ya fasihi ilivyoyashughulikia masuala mbalimbali ya jamii. Mhakiki huyu pia yu mwalimu anayeielimisha hadhira kuhusu kazi za fasihi kwa kuzifasili na kuzichambua kazi hizo akiuweka wazi utata wowote ule unaojitokeza katika kazi hizo. Hapa basi, wakati ambapo mhakiki anakuwa mwanafunzi wa kuelimishwa na yale anayoyakuta katika kazi ya fasihi, hapo hapo mhakiki huyo huwa mwalimu wa msanii mwenyewe na wa hadhira ya kazi ya msanii huyo.

Kwa njia hiyo basi, uhakiki huwa na jukumu la kuidariji kazi ya fasihi na hadhira, na pia huwa kiungo kati ya mhakiki mmoja na mwingine. Mhakiki haiandai tu hadhira kwa ajili ya kazi ya msanii, bali pia humwonyesha msanii namna ya kuendana na wakati na mazingira yaliyomzunguka na jinsi ya *kuilisha* hadhira hiyo vizuri zaidi katika kazi zake zitakazofuatia. Kwa njia hii basi, uhakiki unakuwa chombo kimojawapo cha kuimarisha kazi za sanaa.

*Uhakiki una misingi ya kijamii*, kwa hiyo basi, kinyume na yanayoelezwa katika nadharia tulizozichambua, toka ya Finominolojia hadi ya Hemetiki na Upokezi, ni wazi kuwa kazi za tahakiki ni njia mojawapo muhimu ya kupima na kutathmini masuala mbalimbali ya kijamii.

Nadharia za fasihi na tahakiki zinapoikwepa misingi hiyo ya jamii, hapo hapo hutokea kuathiri baadhi ya kazi za fasihi ambazo kwa kuongozwa na falsafa za nadharia hizo, hukabili masuala ya kijamii kama kwamba ni zao la ombwe tupu lililo nje ya jamii hizo.

**Athari katika Fasihi ya Kiswahili**

Fasihi ya Kiswahili iko katika tarehe mpya. Tapo la Urasimi na Urasimi Mpya kufifia nguvu zake baada ya vifo vya washairi wengi wa rika la Shaaban Robert; na baada ya Ulimbwende na aina mbalimbali za Uhalisia uliozuka katika miaka ya 70 walipojitokeza, miongoni mwa wengi wengineo, washairi huria, ambao pia, kwa namna fulani walitumia masovina kupinga fasihi iliyokuwa imejaa lelemama tu za Uhuru, Mapinduzi ya Unguja na Azimio la Arusha; miaka ya 80 imeleta majaribio mbalimbali katika fasihi hii, hasa katika Tanzania. Wako waandishi kama vile akina Simbamwene, Ganzel, Rutayisingwa, Musiba, Nicco ye Mbajo na Hammie Rajab ambao walijaribu mitindo na maudhui ya kiupelelezi na mapenzi ya kusisimua kiwiliwili tu huku yakibutisha akili. Nia kubwa hapa ni kuvuna magunia ya fedha kwa muda mfupi kiasi iwezekanvyo. Hizi zilikuwa tu ishara za hali ya kuabudu pesa iliyotapakaa katika mfumo wa kibepari wa Tanzania leo.

Kundi kubwa la pili lililoibuka na ambalo hadi leo lina nguvu na athari nyingi ni lile lililotumia kejeli, dhihaka na tashtiti. Waandishi kama vile Gabriel Ruhumbika, Isack Mruma, Harrison Mwakyembe na Paukwa Theatre Association in miongoni mwa vielelezo vizuri vya kundi hili. Kundi hili lilizuka kutokana na hali za kijamii za kukanyagwakanyagwa kwa miiko mbalimbali iliyowekwa na wanajamii wenyewe. Miiko hiyo ilihusu hasa matukio muhimu katika historia ya jamii, hasa ya Mapinduzi ya Unguja ya 1964, Azimio la Arusha la 1967, Mwongozo wa Chama wa 1971 kuhusu uongozi bora, na kuunganishwa kwa vyama vya TANU na AFRO-SHIRAZI ili kuzaliwa Chama cha Mapinduzi (CCM). Matukio yote haya yaliwapa wananchi imani na matumaini ya maisha bora zaidi. Imani hizi zilitokana na miiko na ahadi za matukio hayo. Miiko na ahadi hizo zilipovunjwa waandishi waliamua kutumia mbinu za kubeza, kudhihaki na kuwakejeli wale waliozivunja. Hizi ndizo zilizokuwa mbinu sahihi zaidi hasa kwa vile mambo haya ni masuala nyeti kichama na kiserikali.

Kundi lingine ambalo limejitokeza na tunalolishughulikia kwa kirefu zaidi katika makala ni lile la wanafasihi ambao ama wamejaribu kutumia mbinu za kisanaa za Kiafrika ili kupanua maana za tanzu za fasihi ya Kiswahili ambazo kwa asili si za jadi za Kiafrika, au wamechota kutoka katika mikabala ya nadharia na falsafa kutoka nje na kutumia misingi ya mikabala hiyo kuunda aina mpya ya mwelekeo wa baadhi ya tanzu za fasihi ya Kiswahili. Katika kundi la kwanza tunaweza kuwataja E.N. Hussein ambaye katika *Ngao ya Jadi na Jogoo Kijijini* amechotarisha masimulizi ya ngano kutoka Uganda na Kilwa na ushairi/tamthilia tulizozizoea. Halafu yuko

Penina Muhando ambaye katika *Lina Ubani* na *Nguzo Mama* kafanya majaribio ya kuchotarisha vipengele vya sanaa za maonyesho za Kiafrika na vile vya utanzu wa tamthilia ambao ni mgeni katika fasihi ya Afrika.

Katika kundi la pili la wachotarishaji hao, yumo E.Kezilahabi ambaye uandishi wake wa baadhi ya riwaya, tamthilia na hadithi fupi unaongozwa na uchotarishaji wa falsafa za Kiafrika na zile zisizo za Kiafrika. Kwa vile uchotarishaji huu ni wa wazi zaidi ya ule wa Hussein na Muhando, tutamchambua kwa kirefu zaidi Kezilahabi katika makala hii.

*E. Kezilahabi*

Uchotarishaji katika kazi za E. Kezilahabi ulianzia katika zile za mwanzo za *Rosa Mistika, Kichomi* na *Kichwamaji*. Kazi hizi zinajishighulisha na suala la maana ya maisha kwa kutumia mazingira ya vijiji na miji ya Tanzania lakini kwa jicho la falsafa ya *Udhanaishi (Existentialism),* falsafa ambayo historia yake inaanzia Ulaya kwa wanafalsafa kama vile Soren Kierkegaard, Martin Heidegger na, hasa, Jean Paul Sartre. Udhanaishi huyaona maisha kuwa ni kitu kisicho na maana; ni kitu cha wongo ambacho, kwa hakika, wakati mwingine hakipo bali ni cha kuwazika tu. Tamko la Descartes la *Ninawaza kwa hiyo, nipo* ndilo msingi mkuu wa nadharia na falsafa ya Udhanaishi. Hii ndiyo sababu wahusika wa kazi za E. Kezilahabi, kwa mfano Kazimoto wa *Kichamaji,* Rosa Mistika na Charles wa *Rosa Mistika,* mwishoni wanaamua kuwa maisha hayana maana, kwa hiyo ama wanajiua (Kazimoto na Rosa), au wanaamua kujitenga na uwongo wa maisha hayo kwa kugeuka kuwa baruda (Charles). Ndiyo maana hata katika mashairi yake kama vile ya "Kisu Mkononi", "Nimechoka," na "Dhamiri Yangu" yapatikanayo katika diwani ya *Kichomi* kuna mkabala wa kukatisha tamaa kuhusu maisha. Mkabala huu umepewa muhtasari mzuri katika kipande kimoja cha shairi la "Nimechoka":

> Ukweli wa maisha unakuwa kama ndoto ya uwongo *(uk. 35)*

Ndiyo sababu kwa Kezilahabi, dunia ni uwanja wa fujo na vurugu tupu; fujo na vurugu ambazo mwandishi alivyozichora zinakwepa uhalisi wa misingi yake ya kitabaka.

Kwa ufupi, kutokana na falsafa za nadharia za Udhanaishi, Kezilahabi kaunda maudhui yaliyodhamiria kuonyesha kuwa maisha ni fumbo (RM) lililojaa fujo tupu (DUF) zinazowapa watu vichomi (K) na kuwageuza kuwa vichwamaji (K).

Katika *Rosa Mistika* mwandishi mwishoni ameongozwa na imani ya Kihindu kuhusu *Karma,* kwa kumfanya mhusika anayempendelea kuliko wengine wote, Regina, aendelee kuishi maisha adilifu na mema hata baada ya kufa, kwa kumgeuza kuwa matunda bora ya mchungwa uliopandwa katika kaburi lake la katikati. Matunda haya yanawalisha na kuwapa uhai watoto wa Regina waliosalia duniani.

Ziko riwaya fupi mbili za hivi karibuni za mwandihsi huyu huyu ambazo zinadhihirisha waziwazi athari za nadharia tulizozitaja. Hizi ni za *Nagona* na *Mzingile.* Kwa vile *Nagona* Kielelezo kizuri zaidi cha athari hizo tutaishughulikia kwa kirefu zaidi.

*Nagona* ni riwaya fupi inayolundika mambo mbalimbali ya fani na maudhui yaliyokwisha kuanza kujitokeza katika kazi zingine za Kezilahabi, hasa za *Rosa Mistika, Kichwamaji, Kichomi* na hadithi fupi ya "Mayai Waziri wa Maradhi." Ni kazi ya kiudhanaishi inaoongozwa na nadharia ya udhanaishi na Finomonolojia, nayo yaelekea ilichota kutoka katika visima mbalimbali, hasa vya Kierkegaard, Nietzsche, Heidegger, Jaspers na Jean Paul Sartre.

Mwimo wa msingi wa *Nagona* ambao ni wa kawaida kwa kazi zote za kifinominolojia na kiudhanaishi ni kwamba *hakuna amali timilifu.* Kwa msimamo wa nadharia hizi, kila amali ni yumbifu. Tunamfuatilia mhusika mkuu wa kazi hii ambaye hakupewa jina lolote isipokuwa lile la kimungu la "Mimi", katika safari ndefu aianzayo hata kabla ya hadithi kuanza. Taswira hii ya safari inayomkumbusha msomaji kazi za F. Kafka zenye uelekeo huo huo wa kiudhanaishi, inajengwa katika misingi mikuu mine: *Uhaindani, Uhaipita, Uhainje* na *Uhaindoto.* Njia hizi wakati mwingine zinaingiliana mwandishi anapotumia vionanyuma na vionambele pamoja na mahusiano huria ambayo humtaka msomaji azame katika falsafa, dini, siasa na lugha za Kilatini na Kiarabu kabla ya kuibuka na *baadhi* ya majibu ya mafumbo mbalimbali aliyoyalundika mwandishi katika mtiririko mzima wa *Nagona.*

*Nagona,* basi, ni mchanganyiko wa visasili na uhalisi uliofichwa katika taswira na ishara za mfululizo tangu mwanzo mpaka mwisho. Neno la kwanza kabisa katika sura ya kwanza ni *Yaelekea.* Hili ni dokezo muhimu kuhusu mambo atakayokutana nayo msomaji kwani yote yanaonekana katika ukunguukungu wa matukio ambayo bila kuyasoma mara mbilimbili hayaleti maana ya moja kwa moja.

Tangu mwanzoni mwa riwaya hii fupi, mhusika mkuu anapojikuta katikati ya mji mgeni na wa ajabu, mwandishi anampambanisha msomaji na taswira

na ishara nyingi ambazo zimerudiwarudiwa mno kila mahali, hasa zile za msitu mweusi, paka mweusi, barabara, jogoo, Mimba ya uwezo wa Roho Mtakatifu, Hukumu ya Mwisho na ukichaa. Zote hizi zinaambatanishwa na safari ya mhusika mkuu ambayo twagusiwa kuwa ni ya kuutafuta *ukweli*.

Ghafla mandhari ya hadithi yanabadilika, nasi tunakutanishwa na Babu yake mhusika mkuu ambaye anasaidia kidogo katika kuturudisha kwenye ulimwengu wa uhalisi. Kwa kupitia kwa mzee huyu, mwandishi anatoa ishara moja muhimu sana katika hadithi hii, ishara ya PAA aliyepotea na ambaye inabidi atafutwe. Jukumu la kumtafuta mnyama huyu linakabidhiwa mikononi mwa mhusika mkuu. Katika msako huo tunaweza kung'amua kuwa paa ni ishara ya *wakati* na *uhalisi* wa maisha. Wakati na uhalisi, sawa na mnyama huyu, vina mwendo wa haraka haraka; huonekana kuwa wakati ni mwingi nao umejaa uzuri unaovutia sana na ambao huyadanganya macho ya wanaouishi. Hadithi iendeleavyo, ndivyo hisia inavyoongezeka ya kuwa yupo kiumbe wa ajabu anayemkodolea macho msomaji bila kuyapepesa. Jambo hili limezidishwa kwa kutumiwa kwa dhana ya Kibiblia ya wakati unavyoonekana kwa Mungu, kuwa sekunde moja ni kama miaka elfu, na miaka elfu ni sawa na sekunde moja.

Katika safari hii hii pia yako matukio muhimu mawili. La kwanza ni la kushirikishwa kwa mhusika mkuu katika tambiko la kuitenganisha roho na mwili. La pili ni la kukutanishwa kwa wahusika watatu, Mimi (Ego), Id na Superego. Hawa wanashirikiana katika safari ya kuusaka ukweli. Hawa, katika Saikolojia, huelezwa kuwa wanaunda undani wa nafsi ya mtu, nao wanachangia katika kumfanya mtu ayatambue mazingira yake kwa kuleta maafikiano baina ya urazini wake na uhalisi/ukweli. Safari hii inawafikisha wahusika hawa watatu katika viwanda mbalimbali, kikiwamo kile cha baiskeli zisizo na breki pamoja na cha Nyuklia. Ni hapa ndipo dalili za uhalisi zinaonekana katika *Nagona* zaidi ya sehemu zingine zote zilizojaa maluwiluwi, ndoto na visasili. Sauti ya kejeli na dhihaka inajitokeza hapa kupinga upotezaji wa rasilimali na pesa nyingi katika miradi isiyomsaidia mtu.

Hata hivyo, sehemu hiyo ni fupi mno, kwani, ghafla tunakutanishwa na Babii na Mtume ambao wanaambatana na mhusika mkuu aliyebeba upinde wake na mishale. Hawa huenda wametakiwa na mwandishi wawakilishe dini kuu mbili duniani, Ukristo na Uislamu. Twaonyeshwa kuwa dini hizi hazina nguvu yoyote mbele ya Jitu (kifo), mhusika ambaye twamwona akipiga ukelele wa "Ushindi" mwishoni mwa safari ambayo tumekuwa tukiifuatilia.

Taswira hii ya safari imeunganishwa na ile ya *mviringo*, ambayo mwishoni inakamilishwa na mviringo wa wacheza ngoma mbalimbali wanaoshindania sehemu ya katikati ya huo mviringo. Mviringo hapa unahitajiwa uangaliwe katika kiwango cha ishara za dhana chotara ya maana ya maisha. Hii, zaidi ya kuchanganya mtazamo wa kidhanaishi ambao huieleza maana ya maisha kwa kutumia mviringo na mzunguko, hapo hapo inajihusisha na "Falsafa ya Kiafrika" ilivyoelezwa na watu kama vile Padre Tempels na pia kushirikisha ngoma inayoashiria mwisho wa safari moja na mwanzo wa safari nyingine. Mwanzo na mwisho huu ni fumbo, kwani ni vigumu kuonyesha mwanzo au mwisho wa mviringo.

Katika *Nagona* mwisho wa safari ya Ego, Id na Superego, unakuwa mwanzo wa tarehe mpya, kwani vurugu na makelele ya ngoma yanamfanya Mwanamke ajifungue mtoto ambaye twajulishwa kuwa alikwisha kutabiriwa tangu zamani sana, naye ndiye huyo NAGONA. Ndiye huo ukweli uliokuwa ukitafutwa na wahusika hao watatu.

Kwa kifupi kabisa, hiyo ndiyo hadithi ya *Nagona*, kazi inayotawaliwa na ndoto, maluwiluwi na visasili. Hii ni kazi ya majaribio ambayo inauangalia unafsi na undani wa maisha ya mtu kwa mtazamo wa ki-Heidegger. Uhai, kufuatana na *Nagona*, huweza kueleweka tu katika ishara za ndani ya urazini wa mtu, na si katika nguvu zinginezo za nje. Pale nguvu za nje zinaposhirikishwa, zinatumiwa tu kukejeli na kuyadhihaki maisha.

Sasa basi, jaribio hili lina maana gani, na kwa nini limejitokeza katika wakati huu tulio nao?

Wakati ambapo jaribio la E.N. Hussein huenda linaashiria tu hitima ya utambaji wa ngano na visa vya fasihi simulizi wakati inapozaliwa fasihi andishi ya kitaifa, hitima inayoletwa haraka zaidi na dunia ya leo ya makelele ya redio, televisheni, filamu na video; hili la Kezilahabi linayo misingi tofauti kabisa. Kwa kuelemea mno katika matumizi ya maluwiluwi ya visasili, Kezilahabi anatimiliza tu matakwa ya wimbi la nadharia za fasihi na sanaa zinazojaribu kusisitiza udhhania ambao si wakati wake leo. Akiongelea suala sawa na hili katika makala yake ya "Mythology in Modernist Aesthetics," Alfred Uci kasema yafuatayo:

> The mythological tendency is not imposed upon modernist art by nature and the specific artistic laws, but from the outside, by the needs of the bourgeoisie to mystify the reality, to conceal and camouflage the tidal dramas and conflicts, to disguise and distort their social class sources and causes.[20]

*(Si kweli kuwa mwelekeo wa visasili unajitokeza katika sanaa za usasa, iwe kwa hali ya kawaida au kwa sheria maalumu za kisanaa, bali umelazimishwa kutoka nje na matakwa ya kibepari ya kupotosha ukweli na kuficha vitimbi na migongano pamoja na kukwepa misingi na sababu za kitabaka katika jamii)*

Mwelekeo wa visasili unaojitokeza katika riwaya fupi ya *Nagona* unafunika gubigubi migongano ya kitabaka kwa kumwacha msomaji awe anaelea katika ulimwengu wa ndoto za kubuni. Visasili ni utanzu wa fasihi uliotumiwa na mtu katika hatua zake za mwanzo sana alipokuwa bado hajayaelewa mazingira yake, naye ilimbidi atunge mambo ya kubuni na ya mawazoni tu kuhusu mazingira yake. Hapa ndipo ilipombidi atumie madubwana na mambo ya ajabu ajabu ili kukidhi kiu yake ya kuieleza dunia na mambo yaliyomo katika dunia hiyo. Nafasi ya visasili katika maisha ya mtu leo ni ndogo sana, nayo inajitokeza tu katika jamii za watu ambao bado wamezungukwa na ujinga. Ujinga huu unazidi kufutwa kila uchao na nguvu za kimaendeleo za kisiasa, kitamaduni na kiuchumi. Katika *Nagona* udubwana, uajabuajabu, mambo ya kufikirika tu na ya kubuni hayakutofautishwa na uhalisi, bali tumetakiwa tuyaone yote kuwa ni sehemu ya uhalisi huo. Huu, nionavyo mimi, ndio udhaifu mkuu wa nadharia za udhanaishi, Finominolojia, pamoja na kazi za sanaa zinazoongozwa na nadharia hizo.

Kwa baadhi ya wataalamu wa nadharia za fasihi, inawezekana fasihi hii ya majaribio, hasa ya Hussein (*Jogoo/Ngao*) na Kezilahabi *(Nagona/Mzingile)* ikaonekana kuwa ni juhudi za kupandisha viwango vya kazi za fasihi ya Kiswahili ili kushughulisha vichwa vya wasomaji wenye elimu na utaalamu wa juu wa fasihi na sanaa. Swali kubwa hapa ni: Je, Tanzania na Afrika ya leo ina tatizo la viwango vya chini vya kazi za fasihi, au kubwa zaidi ni la viwango vya chini vya usomaji wa mamilioni ya watu wanaounda hadhira za kazi hizo? Hata kama tatizo ni lile la kwanza, je, utatuzi wake uko katika nadharia na mitazamo ya Umundo, Udhanaishi na Visasili?

**Tanibihi**

1. New York: Norton, 1967
2. Boston, 1901
3. New York na London: Harper, 1930
4. Uk. Wa 4.
5. Kwa maelezo zaidi kuhusu nadharia ya Plato ya suala hili angalia Sura ya Tatu ya kitabu cha F.E.M.K.Senkoro cha *Fasihi na Jamii* (Dar es Salaam: Press and Publicity Centre, 1987) inayoongelea Matapo ya Fasihi.
6. Kitabu hiki ambacho kilitolewa mara ya kwanza mwaka wa 1889 kimedondolewa na Terry Eagleton katika *Literary Theory: An Introduction* (Minneapolis: Univ. of Minnesota Press, 1983)
7. Kama juu, Namba 6, Uk.1.
8. Andiko hili linapatikana pia katika kitabu cha Smith na Parks kilichotajwa juu.
9. Tofauti za matapo haya ya Urasimu Mkongwe na Urasimi Mpya yameelezwa vizuri katika kitabu hicho hicho cha Smith na Parks, na kwa Kiswahili zimeshughulikiwa katika kitabu kilichotajwa hapo juu, Na.5.
10. Kutoka katika kitabu hicho hicho cha Smith & Parks.
11. Hapa nimetohoa tu neon la Kiingereza za *Phenomenology*.
12. Angalia, hasa, Edmund Husserl, *The Idea of Phenomenology* (Dublin, 1969).
13. London: 1962.
14. Neno la Kiingereza lililotoholewa hapa ni *Hermeneutics*.
15. Hiki pia, ambacho kilichapishwa mwaka wa 1960, kimehakikiwa vizuri sana na Eagleton.
16. New Haven, Conn., 1976.
17. Eagleton, Terry, Kama juu, Uk.67.
18. Kati ya kazi mbalimbali za mwananadharia huyu, yafaa kusoma *Das Literarische Kunstwerk* (Poland, 1931).
19. Baadhi kubwa ya mawazo yatolewayo humu kuhusu kitabu hiki cha iser yametokana na uchambuzi wa Eagleton alioufanya katika kitabu chake kilichotajwa juu.
20. Makala haya yanapatikana katika jarida la Albania Today Toleo la 1, Na.38 (1978), Kur. 21-32.

**Marejeo**

Barthes, Roland. *Elements of Semiology*. London, 1967.

Barthes, Roland, *The Pleasure of the Text*. London, 1976.

Baxandal, Lee na Stefan Marowski, Wahariri. *Marx and Engels On Literature and Art*. New York, 1973.

Bennett, Tony. *Formalism and Marxism*. London, 1979.

Bloch, Ernst na wenzake. *Aesthetics and Politics*. London, 1977.

Buck Jr., Philo M. *Literary Criticism*. New York & London, 1930.

Caudwell; Christopher. *Illusion and Reality*. London, 1973.

Eagleton, Terry. *Criticism and Ideology*. London, 1976.

Eagleton, Terry. *Marxism and Literary Criticism*. London, 1976.

Eagleton, Terry. *Walter Benjamin, Or Towards a Revolutionary Criticism*. London, 1981.

Gadamer, Hans-Georg. *Truth and Method*. London, 1975.

Gayley, Charles Mills na Fred Newton Scott. *Methods and Materials of Literary Critics*. Boston, 1901.

Gibbe, A.G.N.M. "Dhima ya Uhakiki," katika *Mulika*, 12, (1978).

Goldmann; Lucien. *The Hidden God*. London, 1967.

Gorky; Maxim. *On Literature*. Moscow, hakina Tarehe.

Heidegger, Martin. *Being and Time*. London, 1962.

Heidegger, Martin. *Introduction to Metaphysics*. New Haven, Conn., 1959.

Hirsch, E.D. *Validity in Interpretation*. New Haven, Conn., 1976.

Hussein, E. *Jogoo Kijijini na Ngao ya Jadi*. Nairobi, 1976.

Huseerl, Edmund. *The Idea of Phenomenology*. Dublin, 1969.

Ingarden, Roman. *The Literary Work of Art*. Evanston, Ill., 1973.

Isser, Wolfgang. *The Implied Reader*. Baltimore, 1974.

Isser, Wolfgang. *The Act of Reading*. London, 1978.

Jameson, Fredric. *Marxism and Form*. Princeton, N.J., 1971

Jameson, Fredric. *The Political Unconscious*. London, 1981.

Jay, Martin. *The Dialectical Imagination*. London, 1973.

Kezilahabi, E. *Rosa mistika*. Nairobi/Arusha/Kampala, 1971.

Kezilahabi, E. *Kichomi*. Nairobi, 1973.

Kezilahabi, E. *Kichwamaji*. Nairobi, 1974.

Kezilahabi, E. *Dunia Uwanja wa Fujo*. Nairobi/Dar es Salaam/Kampala, 1975.

Kezilahabi, E. "African Philosophy and the Problem of Literary Interpretation," Tasnifu ya Ph.D., Chuo Kikuu cha Wisconsin, Madison, 1985.

Kezilahabi, E. *Nagona*. Dar es Salaam , 1987.

Lenin, V.I. *On Literature and Art*. Moscow, 1970.

Lunarchasky, A. *On Literature and Art*. Moscow, 1973.

Lovell, Terry. *Pictures of Reality*. London, 1980.

Mecherey, Pierre. *A Theory of Literary Production*. London, 1978.

Muhando, Penina. *Nguzo Mama*. Dar es Salaam, 1982.

Muhando, Penina. *Lina Ubani*. Dar es Salaam, 1984.

Palmer, Richard E. *Hermeneutics*. Evanston, Ill. 1969.

Senkoro, F.E.M.K. *Fasihi na Jamii*. Dar es Salaam, 1987.

Smith, James Harry na Edd Wienfield Parks. *The Great Critics: An Anthology of Literary Criticism*. New York, 1973.

Voloshinov, V.N. *Marxism and the Philosophy of Language*. New York, 1973.

Wellek, Rene. *Concepts of Criticism*. New Haven & London, 1976.